

Maswali

1. Musa alikaa juu mlimani kwa muda gani?
2. Waisraeli waliuliza Haruni afanye nini?
3. Mbona walitaka sanamu?
4. Haruni alifanya nini kutoka kwa vipuli vya watu?
5. Watu walifanya nini yenye ilikuwa mbaya sana?
6. Mbona Musa alikasirika?
7. Musa alivunja nini?
8. Musa aliwaadhibu watu namna gani?
9. Kabila gani ilikuwa bado inampenda Mungu?
10. Waisraeli walienda kuabudu Mungu wapi?

Majibu

1. Musa alikuwa juu mlimani kwa siku 40.
2. Waisraeli walitaka Haruni awatengenezee sanamu.
3. Walitaka mungu mwenye wanamwona.
4. Haruni alitengeneza ndama ya dhahabu.
5. Watu waliabudu ndama ya dhahabu. Walisahau upendo wa Mungu kwao. Walisema ndama ya dhahabu iliwaokoa kutoka Misri.
6. Musa alikasirika kwa sababu Waisraeli waliabudu ndama ya dhahabu.
7. Musa alivunja mawe mbili iliyoandikwa amri kumi.
8. Musa aliwanyunyiza vumbi ya dhahabu ndani ya maji ya kunywa.
9. Kabila ya Lawi ilikuwa bado inampenda Mungu.
10. Waisraeli walienda Maskani kuabudu Mungu.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 1



22 Ndama ya dhahabu

Kwa Biblia Kutoka 32

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu ni mtakatifu. Lazima tumwabudu Mungu. Tusiabudi kitu kingine chochote.

Somo

Mungu aliambia Musa aende juu ya Mlima wa Sinai ili azungumze naye. Kabla Musa hajaenda juu ya mlima, aliambia Waisraeli watii amri za Mungu wakati wote atakapokuwa huko. Aliwambia ikiwa watakuwa na shida yoyote, Haruni atawashulikia. Aliwambia waabudu Mungu kwa njia walikuwa wameamriwa.

Huko juu mlimani Mungu alizungumza na Musa kwa siku arobaini. Mungu alimwambia Musa kuhusu sheria alizotaka Waisraeli watimize. Mungu alielezea Musa vile alitaka wamwabudu. Mungu alitia Musa moyo. Mungu aliahidi Musa kwamba atawaongoza na kuwalinda kwa muda wote watakuwa jangwani. Mungu alikata mawe mbili iliyo laini kutoka mlimani. Mungu aliandika amri kumi kwa hayo mawe.


Musa alikuwa mlima kwa siku arobaini. Waisraeli hawakuelewa sababu zilizomfanya Musa akae huko kwa muda mrefu. Bunde tu walisahau Mungu. Walisahau kwamba walikuwa wameahidi kuabudu na kutii Mungu.

Waisraeli walimwendea Haruni na kusema, “Lazima Musa amepotea. Lazima amekufia huko juu mlimani. Ni muda mrefu tangu aende juu mlimani. Hatujui nini imemtendelea. Tutengenezee sanamu ili tumwabudu. Hatujui penye Mungu ako wala nini imemfanyikia Musa. Tunataka sanamu tuiabudu.”

Haruni hakukuwa kiongozi mzuri na mgumu kama Musa. Haruni aliogopa kwamba watu watampiga asipowatengenezea sanamu. Haruni aliwambia wamletee vipuli vyao vya dhahabu. Haruni aliyeyusha hivyo vipuli vya dhahabu vyote. Kutumia hiyo dhahabu alitengeneza ndama ya dhahabu. Aliwambia, “Hapa kuna mungu wenu.”

Waisraeli walitaka mungu wanaemuona. Wamsri walikuwa na miungu wengi; walitengeneza sanamu mingi za wanyama na ndege. Waisraeli walitaka mungu kama huyo, mungu wanaemuona. Mungu alitengeneza kila kitu ulimwenguni. Yeye ni mkuu zaidi kuliko vyote vinavyoweza kutengenezwa. Mungu anataka tuwe na imani. Anataka tumwamini hata kama hatumwoni.

Waisraeli walitengeneza madhabahu na kuabudu ndama ya dhahabu. Walifanya vitu vingi viovu. Walisema, “Hii ndama ni mungu wetu aliyetutoa Misri salama.” Lakini Musa hakukuwa amekufa. Mungu aliona vile Waisraeli walikuwa wamemsahau na kuanza kuabudu sanamu. Mungu alimwambia Musa kwamba Waisraeli walikuwa wanaabudu ndama ya dhahabu. Kwa hivyo Musa aliondoka mlimani.



Mataifa mingi za kale
Ziliabudu ndama.

Wamisri waliabudu ndama ndume.
Waliita huyo mungu ndama Apisi

Ndama ndume ilikuwa ishara ya nguvu

Musa alipokuwa akiteremka kutoka mlimani, alisikia kelele na vicheko. Musa alikasirika alipoona Waisraeli wanacheza wakizunguka ndama ya dhahabu. Musa alikasirika sana mpaka akatupa chini hizo mawe mbili za amri kumi. Mawe zilianguka kutoka mlimani na kuvunjika kwa vibande.


Musa aliponda ponda ndama ya dhahabu mpaka ikawa vumbi. Alichukua hiyo vumbi ya dhahabu na kunyunyiza juu ya maji ya kunywa. Waisraeli walipokunywa walikuwa wagonjwa. Hii ilikuwa adhabu kwa sababu ya uovu wao.

Musa alipaza sauti, “ Nani ako upande wa Bwana?” Kabila ya Lawi walikuja upande wa Musa. Wakasema, Tutaabudu Bwana.” Mungu alifurahi kuona kwamba kwa kabila kumi na mbili, moja inampenda. Mungu alichagua kabila ya Lawi kuwa makuhani wake.

Baadaye Musa alienda mlimani tena. Mungu alimpa bao zingine za mawe zilizoandikwa amri kumi.

Mungu alimwambia Musa atengeneze hema la kipekee katikati ya kambi. Hili hema liliitwa Maskani. Maskani ni pahali Waisraeli walilazimika kukuja kuabudia Mungu. Makuhani walifanya kazi maskani.

Hema ya maskani iligawanywa mara mbili. Ndani ya chumba cha ndani Musa aliweka sanduku. Hii ilikuwa sanduku ya dhahabu yenye makerubi ya dhahabu kila upande. Musa aliweka kwa sanduku hiyo mawe ya amri kumi. Sanduku lilikuwa takatifu sana. Uwepo wa Mungu ulionekania kwa chumba cha kipekee kilichokuwa na sanduku. Hiki kichumba kililitwa Patakatifu.



Waisraeli walienda maskani kuabudu Mungu. Walienda kutoa dhabihu ili wasamehewe dhambi. Maskani ilikuwa katikati ya kambi. Ilionyesha Waisraeli kwamba Mungu ako katikati yao. Alikuwa anawalinda. Lazima wakumbuke uzuri wa Mungu na wamuabudu na wamtii.